RIPOTI YA MAENDELEO YA BINADAMU YA TANZANIA (2014)
CONCEPT NOTE

Imewasilishwa kwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Jumamosi 31 Agosti 2013
Pius Msekwa Hall, Dodoma

Dkt. Tausi Kida
Director of Programmes
Economic and Social Research Foundation (ESRF)

Mtiririko wa uwasilishaji:

I. Lengo
II. Uchaguzi na umuhimu wa mada ya Ripoti (THDR 2014)

III. Muundo na mtiririko wa ripoti ya THDR 2014

IV. Mchakato wa kuandaa mada (background papers) kwa ajili ya THDR 2014
V. Kalenda ya kuandaa Ripoti ya THDR 2014

I. Lengo

- Lengo la mada hii ni kuwajulisha waheshimiwa wabunge juu ya Ripoti ya hali ya Maendeleo binadamu ya Tanzania 2014 (THDR 2014): **asili yake, mchakato wa maandalizi** na matarajio yake.

- Lengo ni kuwapa **uelewa juu ripoti hii**, na pia **kuwashirikisha katika mchakato** wa maandalizi yake.

II. Uchaguzi na Umuhimu wa Mada (theme) ya Ripoti THDR 2014

- Mada kuu ya THDR-2014 ni "**Mageuzi ya Kiuchumi kwa ajili ya Maendeleo ya Binadamu**" (*Economic Transformation for Human Development*)

- Mada hii inahusishwa na mahojiano yanayoendelea sasa juu ya **kutokuwa na usawa kati ya kasi ya ukuaji wa uchumi na kupungua kwa umaskini** (Ni muhimu kujitathmini - kwa nini Tanzania, licha ya utendaji wake mzuri kiuchumi, bado jitihada za kupunguza umaskini wa watu wake bado sio za kuridhisha).

- Kupitia mada hii THDR 2014 inakusudia kutathmini kwa kina mahusiano kati ya **ukuaji wa uchumi na umaskini**

- Katika kipindi cha kati ya mwaka 2001 na 2012 **pato la taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 7.3%** wakati **umaskini wa kipato ulipungua kwa asilimia ndogo sana** ; Umaskini wa chakula bado ni 16.6%, Umaskini wa kipato 33.4%

Ukuaji wa Pato la Taifa 2000 -2010



Source: World Development Indicators, 2012

- Wakati takwimu zinaonesha uchumi unakua, kiasi cha wananchi wanaoishi chini ya mstari wa kipimo cha umaskini was chakula bado ni kubwa. (Fig.2).



Hoja thabiti ni kwamba kumekuwa na <u>uhusiano hafifu</u> kati ya mafanikio katika ukuaji wa uchumi na punguzo la umaskini na pia kuna ongezeko la kukosekana kwa usawa katika jamiii (increasing inequality)

- THDR 2014 itafafanua juu ya hoja hii, na hasa dhana kwamba **ukuaji wa uchumi (growth) <u>hauna uhusiano wa moja kwa moja</u> na maendeleo ya binadamu**.

- Sababu nyingine ni ukweli kwamba kwa kiwango kikubwa mwelekeo wa sera na mikakati ya maendeleo Tanzania (kwa sasa) yanalenga zaidi katika kukuza uchumi.
  - Mpango wa maendeleo wa miaka mitano 2011/12 – – 2015/16 (Unleashing Tanzania Growth Potentials)
  - Mpango wa muda mrefu 2011/12 - 2025/26 (Long Term Perspective Plan – Roadmap to Middle Income)
  - Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (Big results Now - BRN)

- Kama lengo **Kuu la ajenda ya maendeleo ya nchi ni ukuaji wa uchumi**, ni muhimu kabisa kuwakumbusha kwamba **maendeleo ya wananchi hayapaswi kusahaulika**.

- Uchaguzi wa mada umefanyika kwa uangalifu na kuzingatia umuhimu wake katika mwelekeo wa sera na mikakati ya kitaifa ya maendeleo kwa wakati huu
- Kwa vile toleo la mwaka 2014 litakuwa la kwanza tumeona ni muhimu lizingatie upana katika sekta zote
- Matoleo yatakayofuata yanaweza kuwa maalumu kwa sekta fulani kwa mfano elimu, afya, mazingira etc kutegemea na umuhimu wake kwa wakati huo.

III. Muundo na Mtiririko wa THDR 2014

Imependekezwa kwamba toleo la THDR 2014 liwe na sura nne kama ifuatavyo:

- Utangulizi **(Preface)**
- **Sura ya 1: Hali na Mabadiliko kuhusu maendeleo ya binadamu** (Status and Progress of human Development)
- **Sura 2: Mageuzi ya Kiuchum i yanayoendelea sasa:** (Economic Transformation in the making: Going beyond growth)
- **Sura ya 3: Mageuzi ya kiuchumi tunayoyataka** (Economic Transformation we want)
- **Sura ya 4: Kuongoza Mageuzi ya kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya binadamu** (Transforming Economic Gains for Human Development)
- **Viambatanisho vya takwimu** (Statistical Annex)

Utangulizi

- Utawafanya wasomaji kuelewa ripoti na kutambua wapi tunatoka na wapi tunakusudia kuelekea

- Utasisitiza **uhusiano** kati ya dhana pana ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya binadamu

Sura ya Kwanza:
Hali Halisi na Mabadiliko Kuhusu Maendeleo ya Binadamu

- ✓ Lengo la sura hii (itajirudia katika ripoti zitakazofuata) ni kueleza kwa ufasaha hali ilivyo kuhusiana na maendeleo ya binadamu Tanzania

- ✓ Itaeleza kilichotokea kuhusiana na maendeleo ya binadamu katika kipindi mathalani cha miaka 20 iliyopita, na hali ilivyo sasa

Sura ya Pili:
Mageuzi ya Kiuchumi Yanayoendelea Sasa

- ✓ Sura hii itafafanua maana ya mageuzi ya kiuchumi, na kinachoendelea katika uchumi wetu kwa sasa
- ✓ Ita tathmini baadhi ya mabadiliko ya kiuchumi ambayo yametokea katika kipindi cha miaka 20 Iliyopita
- ✓ Kwa mfano, Ripoti itachunguza mabadiliko katika pato na mauzo ya nje katika sekta muhimu za kiuchumi kama vile kilimo, viwanda, nishati, madini,utalii na usafiri.
- ✓ Pia kwa sasa kuna baadhi ya maendeleo katika sekta ya gesi ambayo ni ya kusisimua sana. Je kuna Mapengo gani katika sekta hii? na sababu zinazochangia? Muundo wa ajira hapa nchini ni suala jingine la kuangaliwa pia.

Sura ya Tatu:
Mapinduzi ya kiuchumi tunayoyataka

- ✓ Sura hii itaongozwa na matarajio yaliyoainishwa katika Dira ya maendeleo ya Taifa(VISION 2025) suala kuu ni kuelekeza ukuaji wa uchumi endelevu unaohitajika

- ✓ Lengo ni kufikia wastani wa ukuaji wa pato la taifa la asilimia 8-9 katika kipindi cha miaka 15 ijayo kutoka katika kiwango cha asilimia 6-7 cha miaka 10 iliyopita, kwa kutumia ufanisi wa utekelezaji wa mipango wa miaka mitano na ya muda mrefu (FYDP and LTSP)

- ✓ **Ni muhimu sana** lengo hili la ukuaji wa uchumi lichochee ukuaji wa maendeleo ya binadamu

Sura ya Nne:
Kuongoza Mageuzi ya uchumi kwa ajili ya maendeleo ya binadamu

- ✓ Sura hii itakuwa hitimisho la ripoti. - tunahitaji utaratibu imara zaidi kwa ajili ya kuchochea mjadala wa umma kuhusu maendeleo ya wananchi.

- ✓ Kuna haja ya haraka ya kuhakikisha kwamba maendeleo ya wananchi yanapewa kipaumbele katika juhudi za kitaifa za kuinua uchumi (mabadiliko ya fikra, kuweka sera katika vitendo; kuunda taasisi sahihi; kuwa na watumishi wenye utaalamu; kuboresha/kuhimarisha huduma za msingi (mfano Elimu na Afya); Kuboresha miundombinu nk)

- ✓ Lengo ni kuchochea mjadala wa jinsi ya kutafsiri mafanikio ya yanayo patikana katika ukuaji wa uchumi kuelekea katika maendeleo ya wananchi

Viambatisho na majedwali ya takwimu

- ✓Hii ni sehemu ya mwisho ya ripoti
- ✓Itakuwa na takwimu za maendeleo ya binadamu (HDI) kwa Tanzania
- ✓Kiambatanisho kitakuwa na takwimu ya kipindi kirefu cha kati ya Miaka 20 nyuma ili kuonyesha mwenendo na mwelekeo wa maendeleo ya binadamu

(IV) Machapisho (Background Papers) kwa ajili ya THDR 2014

Machapisho 10 (yatokananyo na tafiti mbali mbali) yanaandaliwa na wataalamu kwa ajili ya kusaidia uandaaji wa THDR 2014

Chapisho la kwanza: Hali ya maendeleo ya Binadamu Tanzania

- ✓ Litatoa tathmini ya kitaalamu kuhusu hali ya maendeleo ya binadamu, kuanzia Tanzania ijipatie uhuru mwaka 1961

Chapisho la pili: Mageuzi ya kisera, mabadiliko ya kimuundo na mageuzi ya Kiuchumi Tanzania

- ✓ Lita tathmini fursa na changamoto zinazoletwa na mageuzi ya uchumi , maendeleo ya binadamiu na mabadiliko katika jamii kwa ujumla (social Change)

Chapisho la 3: <u>Kukua kwa Uchumi na Mabadiliko ya kimuundo katika Kufanikisha malengo ya Dira ya Taifa (TDV-2025)</u>

- ✓ Lengo ni kubainisha mahitaji muhimu ili kufanikisha malengo ya TDV 2025

<u>Chapisho la 4: Uhusiano kati ya Kuwekeza katika Maendeleo ya Binadamu na Kukua kwa Uchumi</u>

- ✓ Chapisho hili linakusudia kuonesha uhusiano uliopo kati ya maendeleo ya binadamu na ukuaji uchumi wa muda mrefu – dhana ni kwamba bila maendeleo ya binadamu, ukuaji mkubwa wa uchumi hauwezi kupatikana(na kinyume chake pia ni sahihi)

Chapisho la 5: Ni mbinu/muundo gani unahitajika ili kufikia malengo ya TDV 2025?

- ✓ Lengo ni kuchambua aina gani ya maendeleo ya binadamu yatafanikiwa Tanzania ifikapo 2025 (trajectories) katika mazingira ya mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea kwa sasa. (ukuaji wa uchumi, umaskini haupungui, hakuna ajira za kutosha, nk)
- ✓ Hali kadhalika chapisho litaonesha aina ya ukuaji wa uchumi na mabadiliko ya kimuundo yanayohitajika ili Tanzania isonge mbele kuanzia 2014 kufikia malengo ya TDV 2025

Chapisho la 6: Usimamizi wa Maliasili kwa Kukuza Uchumi Endelevu na Maendeleo ya Binadamu

- ✓ Mada hii inaangalia nini kinaendelea hasa katika sekta ya madini na gesi asilia Tanzania
- ✓ Chapisho litaonesha jinsi gani matokeo yanaweza kutofautiana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kutegemena na jinsi maliasili hizi zinavyo (zitakavyo) simamiwa

Chapisho la 7: Muundo na Kasi ya Kuongezeka kwa idadi ya watu Tanzania

- ✓ Chapisho hili linachambua muundo na kasi ya kuongezeka kwa watu Tanzania kwa kutumia matokeo ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Hii ni muhimu sana mfano katika kutathmini mahusiano kati ya muundo, ongezeko la idadi ya watu na utoaji huduma za msingi

Chapisho la 8: Mageuzi katika Huduma ya Afya Tanzania: Je Malengo yamefikiwa?

- ✓ Chapisho hili litachambua kwa kina mchakato katika utoaji huduma ya afya, yaani mageuzi yaliyotokea katika sekta ya afya katika kipindi cha miongo miwili, na kutathmini kama malengo yake yamefanikiwa au la

Chapisho la 9: Ni nini sababu za kuendelea kushuka kwa kiwango cha elimu Tanzania?

- ✓ Chapisho hili linakusudia kuchambua kwa kina sababu za kuzorota kwa juhudi za kuinua ubora wa elimu Tanzania. Pia litaeleza jinsi ya kurekebisha tatizo hilo kwa ajili ya mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya binandamu siku za usoni.

Chapisho la 10: Hali Halisi ya Maendeleo ya binadamu Zanzibar

- ✓ Chapisho hili litapitia na kuchambua mwenendo na hali ilivyo kuhusiana na maendeleo ya binadamu Zanzibar

- ✓ Chapisho litaonesha hali halisi na kubainisha changamoto na fursa zilizopo kuhusianan na maendeleo ya binadamu katika visiwa vya Zanzibar

(V)Kalenda kwa ajili ya kuandaa Ripoti ya THDR 2014

I. Uchaguzi wa mada ya Ripoti (THDR 2014); Mai – Juni 2013
II. Mchakato wa kuandaa mada (background papers) kwa ajili ya THDR 2014 ; Julai 2013- Januari 2014
III. Uandaaji wa Ripoti ya THDR 2014; Februari – August 2014
IV. Machapisho na Uzinduzi wa Ripoti ya THDR 2014 (September – December 2014)

ASANTENI SANA